# SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Simu: 2133990
Telegramu: Railways
Nukushi: 2133428

Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu
S.L.P 70364
Dar es Salaam
13 Septemba 2018

**HOTUBA YA MKURUGENZI MKUU WA SHIRIKA LA RELI TANZANIA- TRC NDG. MASANJA KADOGOSA KATIKA UZINDUZI WA WIKI YA SHIRIKA LA RELI TANZANIA . NDANI YA WIKI HII TRC IMEPATA FURSA YA KUZINDUA LOGO MPYA YA TRC, PIA WATANZANIA WATAPATA FURSA YA KUFAHAMU MAJUKUM YA SHIRIKA LA RELI TANZANIA - TRC**

Mhe. Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Atashasta nditiye

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Dr Leornard Chamuriho

Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi TRC Profesa John Wajanga Kondoro.

Muwakilishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Dar es Salaam

Mkurugenzi Mkuu wa Bandari - Deusdedit Kakoko

Mkurugenzi Mkuu SUMATRA- Gillard Ngwewe

Wawakilishi wa wadau wa TRC

- Kampuni ya Bakhresa
- WFP
- Kampuni ya YARA
- Wawakilishi wa vyama vya wafanyakazi Trawu na Tamiko
- Uongozi wa shirika la Reli Tanzania
- Pamoja na wafanyakazi TRC

Habari za Asubuhi mabibi na mabwana

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mungu mwingi wa rehema na kutukutanisha hapa leo katika kiwanja cha makao makuu TRC, Dare es Salaam, kwa lengo la kushuhudia tukio la kihistoria kwa wanareli la uzinduzi wa logo ya Shirika la Reli Tanzania.Na uzinduzi huu unaashiria mabadiliko makubwa kufanyika TRC kwa manufaa ya watanzania na maendeleo endelevu ya nchi kwa ujumla.

Wageni waalikwa mabibi na mabwana

Mwaka 2018 umekuwa wa kihistoria kwa Tanzania katika sekta ya uchukuzi nchini hususani usafiri wa reli kufuatia matukio kadhaa makubwa ikiwemo kuundwa kwa Shirika la Reli Tanzania ili kuboresha utendaji, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanya maamuzi ya kuunganisha Taasisi mbili za reli yaani Kampuni ya Reli - TRL na Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli – RAHCO na kuanzisha Shirika la Reli Tanzania - TRC ambalo lilianza rasmi kufanya kazi mwezi Machi, 2018. TRC iliundwa kupitia Sheria ya Reli No: 10 ya mwaka 2017 ili kuendeleza majukumu na kazi zilizokua zikifanywa na RAHCO pamoja na TRL.

Wageni waalikwa mabibi na mabwana

Napenda kuwajulisha Maendeleo ya Miradi inayosimawi na TRC, yaani mradi wa ujenzi ya Reli ya kisasa - SGR na mradi wa uboreshaji wa reli ya kati - TIRP.

Kwa upande wa ujenzi wa reli ya kisasa -SGR yaani “Standard Gauge Railway” (SGR) ina upana wa mita 1.435, Nchi nyingi duniani zilizoendelea kiuchumi, zilitumia reli kuchochea ukuaji uchumi na biashara. Ni kwa sababu usafirishaji kwa kutumia reli una uwezo wa kubeba mizigo mikubwa kwa mara moja, na ni wa gharama nafuu ukilinganisha na aina nyingine za usafirishaji, hasusani kwa mizigo mikubwa na mingi inayokwenda umbali unaozidi kilomita 400.

Wageni waalikwa mabibi na mabwana

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia TRC, imedhamiria kufanya ujenzi wa Reli ya kisasa kwa kiwango cha kimataifa na kueneza mtandao, usiopungua km 2,561 katika kanda ya kati ya usafiri inayounganisha mikoa ya Dar es Salaam/ Mwanza, Kigoma, Katavi na nchi zisizokua na pwani za bandari za Rwanda, Burundi, Uganda na DRC.

Wageni waalikwa mabibi na mabwana

Mradi huu unatekelezwa kwa utaratibu na sanifu na kujenga. Suala la usanifu linafanywa na Mkandarasi mwenyewe na Mradi unagharimiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutekelezwa na Shirika la Reli Tanzania, na mpaka tulipofikia katika ujenzi gharama zinazotumika ni za serikali.

Wageni waalikwa mabibi na mabwana

Mpaka sasa kazi kubwa zinazoendelea ni usanifu, ujenzi wa madaraja, tuta reli, makalaveti, kuzalisha mataruma ya zege, ujenzi wa miundombinu ya ishara na mawasiliano na nguzo za umeme wa SGR. Mataruma ya njia ya reli yanazalishwa nchini katika kiwanda kilichopo Soga, Mkoa wa Pwani katika kambi ya ujenzi wa reli ya kisasa. Kwa siku moja kiwanda kinauwezo wa kuzalisha mataruma 1,080 na kila taruma lina uzito wa kilo 280. Pamoja na hayo utandikaji wa tabaka la kubeba kokoto – reli, kutandika nyaya za ishara na mawasiliano na usimikaji wa nguzo na kupitisha umeme wa kuendeshea treni vitaendelea.

Wageni waalikwa mabibi na mabwana

Mradi unaendelea kutekelezwa katika sehemu mbili za mwanzo zinazojumuisha Dar-Makutopora, kwa lengo kuwa ifikapo 2021 Februari, sehemu hizi mbili za mradi ziwe zimekamilika. Mpaka mwishoni mwa Agosti, 2018, ujenzi umefikia asilimia 22% na mpaka sasa gharama za mradi zinalipwa kutokana na kodi za Watanzania.

Wageni waalikwa mabibi na mabwana

Katika sehemu hizi mbili za ujenzi tunategemea kuwa na stesheni 14 kati ya hizo 10 zina uwezo pia wa kuhudumia treni za mizigo. Stesheni kubwa zitakuwa 3 (Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma) na vituo vikuu 2 vyenye miundombinu, majengo ya karakana, miundombinu ya kuundia treni na huduma za bandari kavu ya Kwala na Ihumwa.

Wageni waalikwa mabibi na mabwana

Ieleweke kuwa ujenzi wa njia ya reli, baada ya kukamilisha madaraja na tuta, tunasuka mataruma ya zege kwa kuunganisha juu yake chuma mbili za reli. Mataruma yanatengenezwa katika kiwanda cha Soga kwa kutumia kokoto, mchanga, saruji na maji inayopatikana nchini. Chuma za reli zinaagizwa kutoka katika kiwanda cha chuma cha NIPPON STEEL cha nchini Japani.

Wageni waalikwa mabibi na mabwana

Kiwanda hiki ni moja ya viwanda vikuu wa vitano (5) duniani vinavyotengeneza vyuma na reli zenye ubora wa hali ya juu. Reli hizi kutoka Japani zimeshawali tangu tarehe 6/9/2018 Bandari ya Daresalaam.

Wageni waalikwa mabibi na mabwana

Inatakiwa mfahamu kwa kushirikiana na TANESCO, zabuni ya kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka gridi ya taifa na kuunganisha kwenye mifumo umeme ya SGR ya umeme wa itakyoendeshea treni, inaendelea ili ukimalizika ujenzi wa mifumo ya SGR, umeme uwepo wa kujaribishia na hatimaye kuendesha miundombinu na mifumo yote ya SGR na hatimaye kutumika katika uendeshaji kwa makadirio kuwa umeme utakaotumika katika uendeshaji wa SGR ni megawati 160.

Wageni waalikwa mabibi na mabwana

TRC inaandaa timu ya watanzania vijana, watakaoajiriwa na kupatiwa mafunzo maalum ili waweze kupokea mifumo hii mipya ya SGR inayojengwa kwa technologia ya kisasa na hatimaye waweze kufanya uendeshaji na matengenezo ya mifumo yote ya SGR.

Vijana hawa wanajengewa uwezo kwa njia ya mafunzo na elimu za vitendo ndani na nje ya nchi. Tumeanza wiki mbili (2) zilizopita,kwa vijana 60 na tunaendelea kutoa mafunzo kwa vijana mia moja (100) ambao ni wahitimu wa shahada mbalimbali zitakazohitajika katika uendeshaji wa mifumo ya SGR.

Mpaka sasa jumla ya vijana 160, wameanza mafunzo ndani ya nchi na baadae wataenda nchi za nje mbalimbali.

Wageni waalikwa mabibi na mabwana

- Kwa upande wa mradi wa uboreshaji  wa reli y kati,wananchi inatakiwa watambue uboreshaji unaofanywa ni uboreshaji mkubwa ambao haujawahi kufanyika tangu reli hii ijengwe na wakoloni nikiimaanisha mjerumani na muingereza ni zaidi ya miaka mia moja(100) .
- Uboreshaji huo utahusisha Kutandika upya njia za reli zenye uzani wa paundi 80 kwa urefu wa kilometa 312
- Kufanya ukarabati wa njia ya reli iliyosalia kwa urefu wa kilometa 658
- Kufanyia ukarabati makaravati  na madaraja 442
- Kuboresha mfumo wa mawasiliano
- Kuboresha vituo vya kupakia na kupakua mizigo vya bandari ya Dar es Salaam, ilala na Bandari kavu ya Isaka.
- Ununuzi wa vichwa vitatu vya treni (vipya) na mabehewa mapya 44 ya mizigo Katika kufikia malengo haya TRC itaingia mikataba 64 kati ya hiyo 32 ni ya kuajiri Washauri mbalimbali, 6 ni ya ujenzi na 24 ununuzi wa vifaa mballimbali na mikataba miwili ni ya huduma. Mpaka sasa zaidi ya 50% ya mikataba hii imeshasainiwa.

Wageni waalikwa mabibi na mabwana

Mpaka sasa tayari wakandarasi wako katika maeneo ya kazi wakindelea na utekelezaji. Katika mradi wa uboreshaji wa reli ya kati utakua na kambi kubwa nne kwa ajili ya shuguli za ujenzi yaani kambi ya kingulwila, Magindu,Kintinku, na Karangasi,  kati ya kambi hizo, kambi mbili zimeanza tayari ujenzi ambazo ni Kingulwila na Mgindu, na kazi rasmi ya utandikaji wa reli itaanza octoba mwaka huu na kwa upande wa kambi zilizobaki ziko katika maandalizi ya awali ya ujenzi wa kambi hizo.

Wageni waalikwa mabibi na mabwana

Mwisho kabisa, Mradi huu umefadhiliwa na Benki ya dunia na kutekelezwa  na Shirika la Reli Tanzania katika kipindi cha muda wa miaka miwili kuanzia juni 2018 hadi juni 2020. Lengo la

uboreshaji wa reli ya kati ni kutoa usafiri wa kuaminika na kukuza upatikanaji wa huduma bora Nchini.

Asanteni sana.

***Imeandaliwa na Ofisi ya uhusiano TRC kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu TRC***

**RELI YETU, MAENDELEO YETU, TAIFA LETU**